

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI
KAZI YA RIKIZO MEI 2020

KISWAHILI III

JINA: _____ **TAREHE:** _____

Jibu maswali yote

Chagua jibu sahihi, kisha uandike herufi yake kwenye mabano.

1. Ndoo _____ imejaa maji.
(a) Hilo (c) Hii
(b) Kile
2. _____ mwalimu alifundisha somo la Kiswahili
(a) Kesho (c) Leo
(b) Jana
3. Kwa kutumia herufi “dh” unaweza kuunda neno
(a) Sikio (c) Dhamana
(b) Theluthi
4. _____ hadhithi kunahitaji umakini mkubwa.
(a) Kusema (c) Kuongea
(b) Kusimulia
5. Nikiwa nyumbani hufanya _____ mbalimbali.
(a) Maneno (c) Miktadha
(b) Shughuli
6. Mama hachoki kunibeba. Jibu la kitendawili hiki ni _____
(a) Kiti (c) Kitanda
(b) Gari
7. Meza, kiti, kitanda, kabati kwa jina moja huitwa _____
(a) Vitu (c) Thamani
(b) Samani
8. _____ utajenga ukuta.
(a) Ukiwa fundi (c) Ukuta ukiwa mbovu
(b) Usipoziba ufa
9. Mama amekula chakula chake. Sentensi hii ipo katika wakati _____
(a) Ujao (c) Mtimilifu
(b) Wa mazoea
10. Mwalimu alitisisitiza tutumie _____ ili kunyosha mistari.
(a) Rula (c) Rura
(b) Lura

Soma sentensi zifuatazo kisha ziandike katika nyakati zilizopo.

11. Wanafunzi huwahi shuleni kila siku

12. Asha alikuja saa mbili asubuhi

13. Shule zitafungwa wiki ijayo

14. Tunafagia darasa

15. Mtoto amemwaga maziwa

16. Andika wingi wa maneno yafuatayo

Umoja

wingi

(i) Habari

(ii) Mzazi

(iii) Mtu

(iv) Jino

17. Tunga sentensi moja(1) kwa kila neno

Hadithi	Mbolea	Kichwa	Wiki
---------	--------	--------	------

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

18. Andika kinyume cha maneno yafuatayo

(i) Rafiki _____

(ii) Cheka _____

(iii) Angamiza _____

(iv) Zama _____

19. Oanisha maneno ya kundi A na maana zake katika kundi B

KUNDI A	KUNDI B
(i) Baba, mama, watoto	A. Mtoto wa mwisho kuzaliwa
(ii) Embe, chungwa, papai, nanasi	B. Wanyama
(iii) Kitinda mimba	C. Familia
(iv) Simba, mbuzi, tembo, paka	D. Ndege
	E. matunda

Kundi A	I	II	III	IV
Kundi B				

20. Tegua vitendawili vifuatavyo

- (i) Nina chemchemi isiyokauka _____
- (ii) Babu amelala ndani ndevu ziko nje _____
- (iii) Zulia la Mungu _____
- (iv) Nikienda kwa mjomba sirudi tena _____

21. Andika kweli ikiwa maelezo ni sahihi au si kweli ikiwa si sahihi

- (i) Wakati uliopo hutumiwa kuonesha vitendo au hali inayotokea wakati huo huo. _____
- (ii) Viumbe hai ni wanyama na mimea _____
- (iii) Kuku na bata ni aina ya ndege _____
- (iv) Kiambishi -“ta”- huonesha mambo yaliyofanyika wakati uliopita.

22. Andika neno ambalo ni sahihi

- (i) Adhabu, azabu , athabu. _____
- (ii) Dhalau, dharau, zarau _____
- (iii) Lura, rura, rula _____
- (iv) Ngombe, ng’ombe, gombe _____

23. Jaza nafasi iliyo wazi

- (i) K__k__mbe
- (ii) Ch__k__la
- (iii) Ub__o
- (iv) D__ftari

Andika methali moja ambayo ungeweza kuitumia kulingana na tukio lililoelezwa hapo chini

24. Mtoto alilelewa vibaya hatimaye akawa jambazi

Methali _____

25. Dereva aliendesha gari kwa kasi na kusababisha ajali mbaya

Methali _____